# HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSOKELO

SHULE YA SEKONDARI KABULA,
S.L.P 592,
**TUKUYU.**

**KUMB. Na. BDC/KBSS/J.INST/2021** 11/12/2020

MZAZI WA MWANAFUNZI
……………………………………….
S.L.P ……………………………….
………………………………………….

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KABULA MWAKA 2021**

## 1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Kabula. Shule hii ipo Halmashauri ya Busokelo kata ya Kabula, ipo umbali wa kilometa 06 upande wa Magharibi kutoka Lwangwa.

Mhula wa kwanza wa masomo unanza tarehe **11/01/2021** unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **11/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **18/01/2021** ndani ya siku saba.

## 2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 **Sare za shule**

**a) Wasichana**

i. Sketi mbili (02) moja rangi ya kijani na nyingine rangi ya kahawia iwe ndefu kupita magoti (mshono ni rinda boksi – yaani marinda mawili tu).
ii. Mashati meupe mawili mikono mifupi ( yawe mapya).
iii. Viatu vya ngozi vyeusi viwili vyenye visigio vifupi.
iv. Soksi nyeupe jozi mbili
v. Sweta moja rangi ya bluu.

**b) Wavulana**

i. Suruali mbili (02) moja rangi ya kijani na nyingine rangi ya kahawia( upana kwa chini ni kati ya sm 10 – sm 15 na iwe na turn up)

ii. Mashati meupe mawili mikono mifupi (Yawe mapya)
iii. Viatu vya ngozi vyeusi viwili vyenye visigio vifupi.
iv. Soksi nyeusi jozi mbili
v. Sweta moja rangi ya bluu.

2.2 Sare ya michezo kwa shule hii ni **Tshirt** rangi ya bluu moja (isiwe na maandishi yoyote) na bukta ya bluu moja ( atavaa siku ya michezo wakati wa michezo tu.)

2.3 **Vifaa vya Darasani**

i. Daftari tisa (09) aina ya counterbook (3 quire). Pia awe na daftari zingine ndogo kwa ajili ya mazoezi yake binafsi.
ii. Rula moja
iii. Mkebe mmoja aina ya oxford.
iv. Kalamu za kutosha.

## 3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka **1978** na kama ilivyolekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka **1995.** Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu na Mafunzo ya ufundi, yenye dhamana ya Elimu Nchini na ofisi ya Waziri mkuu – **TAMISEMI** yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na nakala yake utapewa mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wamafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni jambo la lazima.
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation).
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
i) Kutunza mali za umma

**3.1 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule.**

a) Wizi
b) Uasherati na ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadharika.
e) Kupigana au kupiga
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
g) Kudharau Bendera ya taifa
h) Kuwa mjamzito au kupata mimba
i) Kuoa au kuolewa
j) Kutoa mimba
k) Kugoma , kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
l) Kukataa adhabu kwa makusudi
m) Kuwa na simu ya mkononi

**4.0 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi.**

a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakapo ripoti shuleni.
b) Fomu ya mkataba wa kuchangia chakula iliyosainiwa na mzazi / mlezi.
c) Aje na cheti cha kuzaliwa.

**Tafadhari soma kwa makini maelezo / maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**KARIBUNI SANA KATIKA SHULE HII**

**MWAGENI, A. F**
**MKUU WA SHULE**

**MEDICAL CERTIFICATE FORM**

STUDENT NAME………………………………………………………………………………

To be completed by a Government Medical Officer or a doctor from a recognized health institution in respect of form one entrant. Please examine the above as to her/his physical and mental fitness as a student at this school.

The examination should have to involve the following categories

1. Vision with glasses right ……………………… left……………………………….
2. Blood pressure ……………………………………………………………………
3. Hemoglobin ………………………………………………………………………….
4. F. V. Bleeding ……………………………………………………………………….
5. Urine for sugar. ……………………………………………………………………..
6. Stool for routine examination …………………………………………………….
7. Venereal diseases …………………………………………………………………..
8. Neurosis ……………………………………………………………………………….
9. T. B. Test ……………………………………………………………………………….
10. Any abnormality
    a) Heart ………………………………………………………………….
    b) Lung …………………………………………………………………..
    c) Spleen ………………………………………………………………..
    d) Chest …………………………………………………………………..
11. Is there any serious disease e.g. Leprosy, Epilepsy, Asthma,

    Diabetes ……………………………………………………………….

Doctor's name……………………………………………………….

Signature and official stamp

………………………………….

Date ……………………………….

**FOMU YA MKATABA WA UCHANGIAJI CHAKULA SHULENI.**

Wanafunzi wanaosoma Kabula skondari wanapata chakula cha mchana shuleni kwa wazazi kuchangia chakula hicho. Hili limefanikiwa kwa sababu ya makubaliano ambayo yalifanyika na wazazi wenyewe kukubaliana kuchangia chakula shuleni na kikao cha mwisho mwaka jana wazazi walikubaliana kuendelea kutoa michango ya chakula .

Naomba upokee utaratibu wa uchangiaji na usaini hapo chini kisha utarudisha fomu hii shuleni siku ya utakapomleta mtoto.

1. Mahindi debe 2 kwa mwaka ( zote hutolewa mhula wa kwanza)
2. Maharage ndonya 10 kwa mwaka ( unaweza kulipa awamu mbili)
3. Sukari kilo 2 kwa mwaka (unaweza kulipa awamu mbili)
4. Shulingi 2000/= kwa ajili ya kununua mifuko maalumu ya kutunzia mahindi (Kinga njaa).
5. Shilingi 9000/= kwa mwaka kwa ajili ya malipo ya wapishi, kukoboa na kusaga , viungo na vifaa vya kupikia.
6. Awe na sahani , kikombe na kijiko kwa ajili ya kutumia wakati wa kula.

**JINA LA MWANAFUNZI ………………………………………………………**

**JINA LA MZAZI / MLEZI ……………………………………………………**

**NAMBA YA SIMU YA MZAZI/ MLEZI ……………………………………**

**SAHIHI YA MZAZI / MLEZI……………………. TAREHE ………………..**

|  |  |
|---|---|
| …….............................. | …………................ |
| **NAHASHONI MWANDELILE** | **MWAGENI, A.F** |
| **M/KITI – KAMATI YA CHAKULA** | **MKUU WA SHULE** |